# *Kuna Jambo Lolote Lililo Gumu Sana La Kumshinda Bwana?*

. . .naamini, Bwana naamini,
Mambo yote yanawezekana, Bwana naamini.

2 Na tuendelee kusimama kwa muda kidogo tu kwa ajili ya maombi. Na tuinamishe vichwa vyetu.

3 Baba yetu mwema na mwenye neema, tunakikaribia Kiti Chako cha neema katika Jina la Mwanao, Bwana Yesu, tukiomba rehema kutoka kwenye Kiti cha Enzi. Nasi tunaomba, Baba wa Mbinguni, ya kwamba utatuangalia na kuturehemu, kwamba Wewe utatupatia neema Yako, usiku wa leo. Tusamehe makosa yetu, makosa yetu dhidi ya sheria Yako kuu, takatifu.

4 Nasi tungeomba, usiku wa leo, ya kwamba Wewe ungemkumbuka kila mtu aliye katika Uwepo wa Kiungu. Jalia ujumbe huu mkuu ambao ndio kwanza utolewe, uzame ndani ya mioyo ya kila mtu, kwamba utamwagiliwa maji kwa imani na kuleta mavuno makubwa katika Ufalme Wako.

5 Jalia usiku wa leo, ya kwamba hakutakuwa na mtu mmoja mnyonge miongoni mwetu ibada itakapofungwa, jalia kusiwe na hata mmoja aliye na dhambi zisizosamehewa. Ndipo basi tutakapoenda usiku wa leo kwenye nyumba zetu tofauti, kumalizika kwa ibada, jalia tuzungumze barabarani kama wale waliokuwa wakitoka Emau wakisema, "Je, mioyo yetu haikuwaka ndani yetu, hapo alipokuwa akisema nasi njiani?" Kwa kuwa tunaomba, katika Jina la Yesu, Mwanao. Amina.

6 Mwaweza kuketi. Nilikuwa tu nikiendesha gari kuja huku, niliposikia ujumbe wa mwisho uliokuwa ukitolewa, nami nilisikitika tu kwamba sikufika hapa katika wakati mzuri kusikia mwanzo wake. Nafikiri kwamba tumehubiriwa Injili usiku wa leo.

7 Sasa, kabla tu sijaziita hizo kadi za maombi ambazo hatukuzimaliza jana jioni, ningependa tu kuzungumza nanyi dakika chache juu ya Neno ili kwa namna fulani kuutuliza umati, na kila mtu mahali pake, ili Bwana atubariki, na kuwaponya wagonjwa, na kuwaokoa wale wanaoweza kuokolewa.

8 Nilikuwa, nilienda jukwaani, Jumapili alasiri, nami nilikuwa, nikahisi basi kwamba nilifanya kosa, kwa sababu

nilizungumza baada ya hapo, kwa sababu Ndugu yetu mwenye rehema Tommy Osborn alikuwa ametoa ujumbe.

9 Ndipo mwanangu, Billy, tulipotoka nje, akasema, “Baba, kwa nini ukasema lolote, la zaidi?” kasema, “Roho Mtakatifu alikuwa tu akijaza hicho chumba.” Ndipo basi nilipokuja tena usiku wa leo, jambo lile lile lilitukia.

10 Nami si mhubiri sana, hata hivyo, sikupata elimu ya kutosha kwa ajili ya jambo hilo, lakini Bwana alinipa tu njia nyingine ya kuitangaza Injili Yake, kwa kuwa moyo wangu ulitaka kufanya jambo fulani, nami sikufuzu, labda, kwa njia nyingine yoyote. Lakini nina furaha sana kwamba Yeye huniacha nifanye kile niwezacho kuonyesha kwamba ninampenda, na kumthamini kwa moyo wangu wote.

11 Katika Kitabu cha Mwanzo, mlango wa 18 na maneno manane ya kwanza ya kifungu cha 14, ningetaka kusoma haya:

> Kuna *jambo lililo gumu sana la kumshinda Bwana?*

12 Na sasa, mchezo mdogo tu wa kuigiza kwa namna fulani kuvutia hisia za wasikilizaji.

13 Saa chache kabla hawajakuja kunichukua, vema, nitakaa chumbani, nikiomba, nikingojea. Nafunga milango, hakuna mtu anayenisumbua, nami ninaendelea tu kuomba. Ndipo nilipouhisi Uwepo Wake ukiwa karibu sana, wakati mwingine ninaangalia juu na kuiona, ile Nuru mnayoiona kwenye picha, nazo zimeenea kote ulimwenguni sasa.

14 Halafu nikija mkutanoni napenda kuingia moja kwa moja na kwa namna fulani kuuhisi mkutano, nipate kuona mahali Roho Mtakatifu anaposogea, na ndipo ninaweza kufanyiza mstari wangu wa maombi.

15 Na sasa, tunaona katika sehemu ya kwanza ya mlango huu, Ibrahimu alikuwa ameketi mlangoni pa hema lake kwenye siku yenye joto sana. Hapana shaka ilikuwa siku yenye joto sana, labda malalamiko mengi yalikuwa yakija hivi karibuni kutoka kwa wachungaji wa mifugo, kwamba nyasi zote zilikuwa zimekwisha, nchi ilikuwa inakauka kabisa, na kwamba mifugo walikuwa wanakonda sana, na pia, kwamba upatikanaji wa maji ulikuwa karibu umekwisha kabisa.

16 Walikuwa wamepata mashimo ya maji nchini, na maji yalipopungua, wangechimba, na kuchimba mpaka wafikie mahali ambapo maji yalikuwa yakipenya miambani na bado mifugo hawakuwa na maji ya kutosha kuwanywesha.

17 Mnajua, wakati mwingine wakati mambo yanapoenda mrama, giza, tunajua kwa maumbile kwamba kuna giza zaidi kabla tu ya mapambazuko. Na mara nyingi tunapoona mambo mabaya sana yakitendeka namna hiyo, hasa sana kwa waaminio, hatuna budi kukumbuka jambo hili niani mwetu: kwamba ni Shetani akijaribu kuzuia baraka inayokuja.

18 Ilikuwa hivyo sana katika kisa hiki, Shetani alikuwa akijaribu kuwashawishi wajisikie kwamba walikuwa wametenda mabaya, na alikuwa akijaribu kuzuia ziara ijayo ambayo Mungu angewazuru Ibrahimu na Sara.

19 Nasi tunafundishwa katika Maandiko, ya kwamba mambo yote hufanya kazi pamoja kwa manufaa ya wale wampendao Mungu. Haidhuru linaonekana baya jinsi gani, kumbukeni, halina budi kuwa likifanya kazi kwa manufaa yako. Nina furaha sana kwa jambo hilo.

20 Shetani amekuwa akinifuatilia siku nzima, kwa hiyo ninaamini tu ya kwamba Kuna baraka iliyowekwa akiba hapa katika jiji hili, mahali fulani. Nami najua, wakati anapojaribu, na kujaribu kuzuia, anajaribu kufanya nini? Kuwafanya msiamini. Na kama wewe. . .Jambo baya sana unaloweza kufanya ni kutokumwamini Mungu. Na mara unapopata hofu kidogo, "Vema, labda sijafanya *hili*, na sijafanya *lile*," papo hapo, Shetani amekunyang'anya baraka hiyo. Huwezi kuifikia mradi Shetani anakufanya uwazie hivyo.

21 Na labda, kama tungesikiliza mambo kama hayo ya majaribu kama hayo, na kuyazingatia, basi ingekuwa kwamba tungeikosa baraka.

22 Laiti ningalikuwa na wakati, kiko niani mwangu sasa, kisa kimoja maalum cha jinsi ambavyo nisingeweza kupata mahali pa kuombea. Mungu alionekana kuniongoza kuingia nyikani. Basi huko chini kabisa Indiana ya Kusini, ambako maskini msichana mmoja alikuwa amelala kwenye kitanda cha mateso, naye, alikuwa na kifua kikuu, wala hata hakuwa ameinua kichwa chake kutoka kwenye mto kwa muda wa miaka tisa na miezi minane. Alikuwa mfuasi wa kanisa ambalo halikuamini katika uponyaji wa Kiungu.

23 Na wakati huo, nilikuwa tu nimeanza mzunguko wangu, Kanisa la Kibatisti la Milltown. Nikiwa mhudumu wa Kibaptisti, vema, nilikuwa nikihubiri kwa mzunguko, nami nilikuwa nimelijumuisha kanisa hili, naye Bwana alikuwa akifanya mambo makuu.

24 Nao wakaniita nije kumwombea maskini msichana huyu, mwenye umri wa kama miaka kumi na saba, naye alikuwa mahututi sana. Ndipo yule ndugu mwema aliyekuwa amenipeleka kule. . .Baba yake alikuwa shemasi katika kanisa fulani hili ambalo halikuamini katika uponyaji wa Kiungu, nalo lilikuwa limetoa kauli kwamba kama yeyote wa washiriki angehudhuria kanisa la Kibaptisti ambako nilikuwa nikiwaombea wagonjwa, angetengwa na kanisa. Baba yake, akiwa she—shemasi, kwa namna fulani lilimweka katika hali ngumu sana.

25 Kwa hiyo, nitaufupisha tu upesi niwezavyo. Basi nakumbuka, nilienda kumwona huyo msichana mdogo. Mama

yake akatoka chumbani, naye baba yake alikuwa ameondoka nyumbani, kwa maana wasingekuwa na uhusiano wowote nalo. Lakini maskini msichana huyo alikuwa amesoma kitabu nilichokuwa nimeandika kiitwacho, *Yesu Kristo Yeye Yule Jana, Leo, Na Hata Milele.*

26 Ndipo nilipoingia chumbani, asingeweza hata kuinua mikono yake kushikilia kikombe chake cha makohozi apate kutema mate wakati akikohoa. Alikuwa na uzito wa ninii, kadiri ratili thelathini na tano, ama arobaini, maskini miguu yake ilikuwa tu na ukubwa *huu*, mwembamba sana kuliko Florence Nightingale kwenye picha ile, ambaye aliponywa kansa.

27 Nami nikamwombea, naye akaniuliza kama mimi... ataweza kutembea kama yule msichana mdogo wa Kimethodisti ambaye alikuwa amelemaa kwa muda mrefu sana, jina lake Nail. Nami nikasema, "Dada, Malaika wa Bwana alikuwa amesema nami na kuniambia niende katika nchi hiyo, na kumtafuta msichana huyo." "Vema," nikasema, "sijui."

28 Baada ya ule uamsho wa majuma mawili, nikija tu kanisani, mhudumu mpya, tulikuwa na ibada ya ubatizo huko juu mahali panapoitwa Totten Ford alasiri hiyo nilipokuwa nimewabatiza watu mia moja na hamsini majini. Ndipo nikaenda kula chakula cha kutwa pamoja na baadhi ya marafiki zangu, rafiki yangu wa zamani, jina lake George Wright. Ndipo Kitu fulani kikaanza kunisukuma, kikisema, "Panda uende nyikani ukaombe." Vema, kamwe nisingeweza kukiondoa akilini mwangu.

29 Sasa, wakati kitu chochote kinapokusukuma namna hiyo, nenda ukifanye mara moja, maana ni Roho Mtakatifu. Sasa, angalia kitu cha kukizuia.

30 Ndipo Bibi Wright akasema, "Ndugu Billy, nitakapopiga maskini kengele ya bara ya chakula cha kutwa..." Sidhani mnazo hapa Oklahoma, lakini huko nyuma, wangepiga kengele, ni nchi ya milima, nao wakulima wanaweza kusikia kengele hii ikilia kisha watakuja kwenye chakula chao cha kutwa. Naye akasema, "Nitakapopiga kengele, chakula cha jioni kiko tayari," kisha akasema, "basi utakuja uingie, na uwe tayari kurudi kanisani usiku wa leo." Ibada ya uamsho ilikuwa inamalizika wakati huo.

31 Nami nikasema, "Vema, Dada Wright." Nikapanda juu ya kilima, nami nikaanza kupiga magoti, nao waridi mwitu ulikuwa ukinichoma. Vema, nikasogea mbele kidogo, nayo ardhi ilikuwa ngumu sana, hayo mawe, nisingeweza kabisa kutulia, hayo mawe. Nikazunguka kando ya kilima, nacho kilikuwa kimeinama upande mmoja kupita kiasi, na, mwajua, ibilisi akijaribu tu kukuzuia usipate baraka, hivyo tu ndivyo ilivyokuwa.

32 Ndipo nikapanda juu kidogo kichakani, nami nikapiga magoti, m—mbu walikuwa wakivuma kila mahali masikioni

mwangu, ndipo ikawa vigumu sana kwangu kuomba. Ndipo nikaamini basi ilikuwa ni ibilisi, kwa hiyo nikasema, "Ee Bwana Mungu, unirehemu." Basi nikaitupa tu mikono yangu juu na kuanza kuomba, kwa vyovyote vile, na kuwaacha tu mbu washibe wakitaka.

33 Lakini kulikuwa na jambo fulani lililokuwa mzigo moyoni mwangu. Basi baada ya kuzama sana katika maombi. . . Nadhani ninyi Wakristo mnajua maana ya kuzama katika maombi, kusahau tu mahali ulipo, huko ni kuomba katika Roho, naamini. Nami nikafungua macho yangu, na kando tu ya kichaka kidogo cha dogwood, kulikuwako na ile Nuru ikining'inia pale, na Hiyo, Nuru ikiangazia mahali nilipokuwa, Yeye akasema, "Amka, uelekee kwa njia ya Carter."

34 Vema, nilipoangalia pande zote, giza lilikuwa karibu kuingia, kengele ilikuwa ikilia, nao walikuwa na vikundi vya watafutaji vinanitafuta. Nikaruka juu na kukimbilia msituni upesi sana, nami nikaruka juu ya waya mdogo wa seng'enge, moja kwa moja mikononi mwa Ndugu Wright.

Akasema, "Ndugu Billy," akasema, "Mama amekuwa akipiga kengele hiyo, nasi tumekutafuta kila mahali."

Nikasema, "Ndugu Wright, hakuna chakula cha jioni, maskini Georgia Carter atatoka kwenye kitanda hicho na kuishi."

Naye akasema, "Unajuaje?"

Nikasema, "Bwana alikutana nami moja kwa moja pale karibu na kichaka cha dogwood na kuniambia nielekee kwa Carter."

35 Mnaamini Mungu hujibu pande zote mbili za mstari? Mama yake. . .Alasiri hiyo, maskini Georgia alitaka kubatizwa sana, hata alikuwa amelia alasiri nzima. Naye mama yake, mwanamke mzuri, nitawapa anwani yake kama mngetaka kumwandikia baada ya hapa, naye mama yake, mwanamke mzuri sana, baba yake, pia. Nao wanaishi kwa namna fulani ukingoni mwa mji huo mdogo. Na kwa hiyo, alikuwa amelia alasiri nzima. Mama yake, kijana, hata hivyo alikuwa ameingia mvi kutokana— kutokana na kuketi tu kwa miaka tisa kando ya msichana huyo, akimwangalia akififia na kufa.

36 Hakuwa ameona majani, wala nyasi, wala chochote kile kwa muda wa miaka tisa na miezi minane, aliyokuwa amelala kichalichali. Wasingeweza hata kumweka kwenye maliwato ya kitandani, alikuwa na shuka la mpira chini yake, nao wangevuta tu hilo shuka, shuka la—la kitani ya kawaida. Ndipo basi alikuwa akilia, na kutaka kupata nafuu apate kwenda na kubatizwa.

37 Na kwa hiyo alasiri hiyo tulikuwa tumembatiza msichana wa Nail aliyekuwa amelemaa kwa—kwa kiharusi kwa, loo, muda

mrefu, ama ilikuwa yabisi kavu, ilimlemaza na kuupinda mguu wake, basi alikuwa mzima tu kama msichana mwingine yeyote. Naye alitaka kubatizwa pamoja na msichana wa Nail.

38 Naye mama yake alikuwa amevunjika moyo sana hata akahamia jikoni, kumsikia binti yake mwenyewe akilia na amelala pale akifa, naye akainua mikono yake, na kusema, "Ee Bwana Yesu, laghai yule amepitia katika nchi hii na kumdhoofisha sana mtoto wangu na kumfadhaisha sana." Kisha kasema, "Huyo hapo maskini mtoto huyo, amelala mle ndani akifa, halafu yeye anakuja huku na kusema kitu kama hicho, na kumfanya alie, na—na kadhalika."

39 Basi wakati alipokuwa akiomba, sasa hii ndiyo hadithi yake, siwezi kusema hii ni kweli, ila tu naamini ni kweli, akasema, aliona kivuli kikija kupitia ukutani, naye akafikiri ilikuwa ni binti yake aliyeishi milango michache chini yake, akija kumwona nyumbani, basi alipoangalia juu, alisema ilikuwa ni kivuli cha Yesu ukutani.

40 Naye akasema, "Ni nani *huyu*?" na kuelekeza kidole upande *huu*, naye akaona, kama ono, akiona paji la uso wangu mrefu hapa, nikiingia, nimebeba Biblia juu ya moyo wangu. Naye akaruka mbio kumwambia binti yake, na yapata wakati huo nilikuwa nikiingia mlangoni. Mungu daima anakuweka hapo kwa wakati unaofaa, kama tu utaamini.

41 Marafiki zangu wa thamani, nikaenda kitandani, na kusema, "Georgia, sijui ni kwa nini, lakini Yesu Kristo," nikaangalia nyuma ya kitanda chake ambapo wakati angeweza kurudisha mikono yake nyuma, alikuwa amesugua rangi yote kutoka kwenye hicho kitanda kidogo cha bango ambapo maskini mikono yake ilikuwa huko nyuma, akilia na kulia na kuomba, na kusema, "Georgia, Yesu Kristo, anakuponya, simama kwa miguu yako."

42 Sijui ni kwa nini nililisema. Kwa nafsi yangu, nisingesema hilo bure, kwa sababu msichana huyo atasimamaje wakati miguu yake si mikubwa *hivi* pajani? Nayo maskini mikono yake, hata asingeweza kuinua mikono yake juu kuchukua kikombe chake cha makohozi.

43 Sasa, huenda ukamwuliza mama yake, na umwache akupe taarifa ya daktari juu yake. Naye... basi wakati yeye... Nikamshika mkono, na rafiki vipi? Sijui, siwezi kusema, bali hakuna lililo gumu sana asiloliweza Bwana, ndipo msichana huyo akaruka kutoka kitandani kwa vijiti hivyo vidogo vya miguu alivyokuwa amesimamia, nami nikageuka nimejawa sana na Roho Mtakatifu, nikatoka mlangoni.

44 Na katika dakika chache yeye, mama yake akazimia, akipiga mayowe, watu wakaanza kukimbia kutoka kila mahali, naye Georgia akatoka nje, jina ni Georgia Carter, akatoka nje na alikuwa akibariki nyasi na majani juu ya miti, mara ya

kwanza alipokuwa ameyaona katika miaka tisa na miezi minane. Naye. . . Watu walikuwa wakimshughulikia mama yake, maana alikuwa amewazia ya kwamba alikuwa ameaga dunia.

45 Na—naye Georgia akakimbilia mahali pale, wakati aliposhikwa na TB, alikuwa akijifunza piano, ama kinanda, hasa, naye alikuwa ameketi kwenye kinanda akikipiga. Ndipo baba yake akasikia kelele hizo, naye akakimbia kutoka ghalani, akija kuona shida ilikuwa ni nini, akileta kopo dogo la maziwa, ndipo akaingia mbio mlangoni, na alipoingia, huyo hapo binti yake ameketi kwenye kinanda akicheza:

> Kuna Chemchemi iliyojaa Damu,
> Iliyotolewa kwenye mishipa ya Imanueli,
> Ambapo wenye dhambi wakitumbukizwa chini ya hiyo gharika,
> Wanapoteza madoa yao yote ya hatia.

46 Sasa, jina lake ni Georgia Carter, C-a-r-t-e-r, Georgia Carter, Milltown, Indiana. Mwandikie, kama ungetaka kupata huo ushuhuda wewe mwenyewe.

47 Halafu basi, hilo linakuonyesha ya kwamba wakati Shetani anapojaribu kukuzuia kupata kitu kilicho sahihi, endelea kusonga mbele, haidhuru.

48 Sasa, Shetani alikuwa akijaribu kuwazuia Ibrahimu na Sara, kwa sababu alijua ya kwamba ziara ya Malaika ilikuwa inakuja.

49 Ndipo basi wakati kila kitu kinapoinuka, yote nje ya utaratibu, basi tunajua kuna kasoro fulani. Sasa, ninaamini, labda kama tungemsikiliza Shetani, huenda tukakosa kuliona, kama Sara alivyofanya.

50 Hebu tuwazie ya kwamba Sara, kwa kuwa alifanya yale aliyofanya, hebu tuwazie ya kwamba kwa namna fulani alikuwa mwenye ugomvi kidogo asubuhi hiyo, hata huenda alisema, "Ibrahimu, unajua tunapungukiwa na vitu hapa, nao wachungaji wa mifugo wanasema ma—malisho yote pamoja na mashimo ya maji yamekauka, nafikiri ulifanya uamuzi mbaya ulipochagua kuja huku, na kumwacha Lutu na Bibi Lutu na familia yao waishi huko chini wakiwa na mali nyingi.

51 "Mbona hivi majuzi, ama wakati fulani uliopita, hasa, nilipoenda mjini, mbona, Bibi Lutu alikuwa amevaa moja ya nguo nzuri sana nilizopata kuona, mtindo wa Wamisri. Mbona, msafara wa ngamia ulipita, naye akapata mitindo mipya. Hakuna vitu kama misafara na mitindo kupitia pande hizi."

52 Lakini laiti angalijua tu, kulikuwa na zaidi ya msafara uliokuwa ukipita, kulikuwako na jeshi la Bwana likija upande huo!

53 Na huenda nilimsikia akisema kitu kama hiki: "Unapaswa kuona mtindo mpya wa nywele aliokuwa nao." Mwajua, mwanamke mwenye umri wa miaka sitini, akijaribu kuonekana

wa ishirini. Lakini hayo ni mambo tu yanayovutia usikivu wako, kitu fulani, kutoka kwa mambo ya Mungu, hilo ndilo ninalojaribu kufikia. "Laiti ungalimwona."

54 Basi maskini mzee Ibrahimu, ndugu mzee mwaminifu, mimi. . .hilo halikumtikisa hata kidogo, anaenda tu pale na kuchukua kiti chake na kuketi chini mlangoni pa hema. Ninapenda hilo.

55 Mliona, wakati Malaika walipomjia Lutu, Lutu alikuwa ameketi langoni, lakini Ibrahimu alikuwa ameketi mlangoni? Lango linaelekeza uani, lakini mlango unakuingiza ndani ya nyumba. Ninapenda kuketi mlangoni, madhabahuni, karibu sana Naye niwezavyo, hapo ndipo palipo na matarajio yangu, madhabahuni, nikingojea kuonekana Kwake.

56 Ibrahimu anachukua kiti chake na kuketi chini, basi mwangalieni maskini mtumishi mwaminifu wa Mungu akiinamisha kichwa chake, na labda Sara, mwenye ugomvi kidogo na kuendelea, lakini aliyaacha tu yaendelee, akaanza kukumbuka, "Ni baraka ngapi kuu ambazo Mungu amenipa!"

57 Mnajua, wana wa Mungu wanaongozwa na Roho wa Mungu. Mnaamini hilo? Ndipo alipokuwa ameketi pale, akiwazia juu ya wakati ambapo Mungu alimtokea katika Jina la Mwenyezi, yule El Shaddai (kifua, matiti ya mwanamke), Mpaji-Nguvu. . .

58 Sasa, mkiangalia hilo neno ni neno ambatani, ambalo linamaanisha, *Shaddai*, sio "titi," bali, "mwenye matiti," mawili. "Alijeruhiwa kwa makosa yetu; kwa kupigwa Kwake sisi tuliponywa." Loo, nina furaha sana kwa jambo hilo! Ama—ama ahadi ya kifua cha Mungu, Yeye ndiye Mwenye Nguvu, Mpaji-Nguvu. Kama wewe. . .

59 Ibrahimu, mzee, mwenye umri wa miaka tisini na tisa, alisema, "Ibrahimu, mimi ni Mungu mwenye matiti. Shikilia tu ahadi Yangu, na unyonye nguvu zako kutoka Kwangu." Hivyo ndivyo ilivyo kwa kila mwaminio atakayelichukua Neno la Mungu, wala usilitilie shaka, bali lishikilie tu na kunyonya nguvu zako.

60 Ni kama mtoto mchanga, anayelala kifuani mwa mama, wakati wote anaponyonya, ameridhika. Wakati Mkristo halisi anapoweza kushika ahadi ya Mungu, na kuamini ni kwa ajili yao, ameridhika wakati anaponyonya nguvu zinazokuja. Hatalalamika hata kidogo, ameridhika tu. Loo, ninapenda utoshelevu huo wa kujua ya kwamba Mungu alisema hivyo.

61 Wakati yule mtakatifu mzee alipokuwa ameketi pale ameinamisha kichwa chake, bila shaka akiomba, hapo ndipo alipoinua kichwa chake na akaona Watu watatu wakija kuelekea kwenye hema. Loo, akaruka upesi, hapana shaka ilikuwa ni Roho, aliyesema, "Waendee."

62 Mwajua, kuna kitu fulani kuhusu watu waliojazwa na Roho ambacho kinatambua Uwepo wa Mungu. Sijui ni kwa nini, lakini lazima iwe kwamba wao—wao wana kitu fulani ndani yao kinachowavuta kwa sumaku kwa huyo Roho wa Mungu. Ndipo akatambua ya kwamba kulikuwa na kitu fulani.

63 Hata Lutu, katika hali yake ya kurudi nyuma, wakati wale Malaika wawili wa kiinjilisti, wajumbe, wainjilisti, ama chochote unachotaka kuwaita, waliposhuka kule, Lutu, akiketi langoni, cheche ndogo ingali ilikuwa imesalia moyoni mwake. Alitambua ya kwamba ilikuwa ni Malaika, ilikuwa ni wajumbe kutoka kwa Mungu.

64 Wakati Ibrahimu alipoenda kuwalaki, aliwaweka kando, na kusema, "Ingieni mketi chini, ketini chini ya mwaloni kwa muda kidogo, na hebu nilete maji kidogo mkaoshe miguu yenu, nami nitawapa kipande cha mkate. Halafu mpumzike tu kidogo, ndipo mnaweza kwenda zenu."

65 Loo, alipomweka chini pale, ingawa hawakuonekana tofauti na watu wengine wowote, kwa sababu walikuwa wamevaa nguo, mavumbi nguoni mwao na walitoka Nchi nyingine, labda miguu yao imejaa mavumbi na nguo zao zimechakaa, lakini Ibrahimu alijua mle ndani, kulikuwa na kitu halisi. Roho alilitangaza. Kwa nini? Alijiweka katika mazingira ya kiroho wakati wote, hata angeweza kutambua mema na mabaya wakati wote.

66 Hivyo ndivyo Mkristo anavyopaswa kufanya siku hizi, ni kujiweka katika maombi, chini ya mazingira ya kiroho, sikuzote. Pasipo kutazama u—upande mbaya, akiangalia upande mzuri. Ninyi ni watoto wa Mungu, mnaotarajia baraka Zake.

67 Baada ya kuwasimamisha, ninaweza kumwona akiingia ndani mbio na kuunyakua mkono wa Sara, na kusema, "Njoo kando, Mpenzi, kidogo tu. Nataka kukuambia jambo fulani, ninaamini tunapata siku yetu ya kujiliwa sasa hivi."

68 Huyo akatoka akapitia kwenye kundi, akamchukua ndama mdogo na kumtayarisha, akamtoa nje na kuwalisha hao watu. Wawili wao wakainua vichwa vyao wakaelekea mahali walipokusudiwa kuhubiri Injili kwa nchi hiyo iliyopofushwa na mahubiri yao.

69 Jinsi tunavyopaswa kuwazia siku hizi, ya kwamba kuhubiriwa kwa Injili humpofusha asiyeamini. Si ajabu hawawezi kuona, wamepofushwa. Mungu anasema wana macho, wala hawawezi kuona, masikio wala hawawezi kusikia.

70 Mungu, kama kuna jambo lolote ninalotaka Yeye anifanyie, ni kuyafungua macho yangu ya kiroho nipate kumtambua na kuangalia pande zote na kumwona, kwa kuwa Yeye yuko kila mahali. Ninataka kumwona na kumfahamu sana hata nitamjua nitakapomwona kwa mara ya kwanza kabisa, nitatambua ya kwamba ni Mungu. Hiyo ndiyo shauku ya moyo wangu: Kuwa kama Ibrahimu alivyokuwa.

71 Basi kumbukeni, tukiwa tumekufa katika Kristo, sisi ni Uzao wa Ibrahimu. Naye Ibrahimu aliwatambua watu hao walipokuwa wakija kuwa ni wajumbe wa Mungu, kwa kuwa jinsi alivyowatendea, ilithibitisha ya kwamba alijua ya kwamba walikuwa ni wajumbe wa Mungu.

72 Na baada ya hao wengine wawili kwenda mahali walipokusudiwa kuhubiri Injili, Huyu Ambaye alimwita Bwana. . . Na hiyo *Bwana* ni herufi kubwa B-w-a-n-a, "Elohimu," Yehova Mkuu, Mwenye Nguvu, Yeye alikuwa katika mwili, Mwanadamu.

73 Mtu fulani aliniambia wakati fulani uliopita, kasema, "Sasa ngoja kidogo, Billy, kweli huamini ya kwamba huyo alikuwa ni Mungu?"

Nikasema, "Hakika ninaamini alikuwa ni Mungu."

Kasema, "Mungu angewezaje kamwe kuwa katika umbo la mwanadamu?"

74 Nikasema, "Vema, huenda ukafikiri ilikuwa ni Thiofania, bali sivyo, kwa sababu Yeye alikula nyama ya ndama, akanywa maziwa, akala ugali, akaketi pale, akazungumza, Yeye alikuwa ni Mwanadamu. Mungu alikuwa akionyesha jambo fulani."

75 Loo, mbona ni rahisi kwa Mungu wetu kunyosha mkono na kuchota konzi ya kalisi, potashi, na petroli, tumeumbwa kwa elementi kumi na sita mbalimbali za ulimwengu, alifanya elementi zote, anyoshe tu mkono, na kunyakua konzi ya elementi, aseme, "*Whiu!* Ingia katika huo, Gabrieli." Aunyoshe tena na kuchota nyingine, "*Whiu!* Ingia katika huo, Mikaeli." Ajichotee Mwenyewe nyingine, "*Whiu!*" Aingie humo ndani.

76 Mbona hakika, Yeye ataniita siku moja, na huenda nisiwe—nisiwe zaidi ya hilo, Naye ataniita niurudie mwili wangu tena katika ufufuo. Tunaye Mungu Mwenye Nguvu kama Mungu wetu. Hakika, ninaamini ilikuwa ni Yeye. Na kisha atoweke asionekane tena, aliutumia tu huo kadiri alivyotaka, kisha akaurudisha tu mavumbini tena; Yeye atakutumia kadiri apendavyo, kisha akurudishe mavumbini; Yeye atanitumia kadiri atakavyo, kisha nitarudi mavumbini. Lakini loo, wazo hilo tukufu, na ukweli huo mtukufu kwamba siku moja Yeye ataita nasi tutafufuka kutoka mavumbini! Tunaitazamia saa hiyo.

77 Naye Huyu hapa sasa, naye Sara, "Mimi," hebu na tumwingilie tu kwa dakika moja, huyo hapo ameketi kule nyuma, kasema, "Nashangaa kwani mume wangu anaweza kuwakaribisha walokole wangapi?" Naye huyo hapo ameketi huko nje, mwajua, naye Ibrahimu anavutiwa tu, labda maskini kifukuza nzi, mwajua, akiwafukuzia mbali nzi, na kusema. . .

78 Vema, ninamwona Malaika akichukua kiti Chake, labda, na—na kuegemea upande, mgongo Wake umeelekezwa kwenye

hema. Naye Sara akisikiliza kupitia hemani, mwajua, kidogo akisikiliza kisiri, mwajua, na kusikiliza kupitia hemani. Naye kwa namna fulani alikuwa na hisia mbaya sana asubuhi hiyo.

79 Huoni mambo unapokuja kanisani na hisia ya namna hiyo. Wewe tu, hakuna haja ya kujaribu, afadhali ungalikaa nyumbani, hutapata chochote kutoka kwake. Nenda nyumbani katika . . . Unapokuja kanisani, njoo umeomba, njoo kwenye mazingira, njoo ukitarajia.

80 Ibrahimu alijua ya kwamba wakati wa ile ahadi ulikuwa unakaribia, ilibidi iwe, alikuwa na umri wa miaka mia moja. Alikuwa akiitarajia wakati wowote, aliangalia kila dakika. Alipoingia mbio, alimwambia Sara, "Hii, naamini, ndiyo siku yetu ya kujiliwa."

81 Naye kwa namna fulani akamtazama kwa hayo macho makubwa, na kuwazia, "Vema, Ibrahimu, umesema hivyo muda mrefu." Lakini unajua, utakuja wakati ambapo itakuwa hivyo, kama Mungu alisema hivyo.

82 Ndipo yule Malaika akachukua kiti Chake na kuegemea nyuma, Yeye akasema, "Ibrahimu, kwa kuwa umepata kibali kwa Mungu, kwamba wewe ni mrithi wa ulimwengu, na—na utakuwa baba wa mataifa mengi, nawe umeamini hilo tangu ulipokuwa na umri wa miaka sabini na mitano," miaka ishirini na mitano, vinginevyo "umemngojea mtoto huyu aliyeahidiwa kwa Sara, na sasa, sitawaficha hili, kile nitakachofanya, nitakurudia, kwa muhula wake."

83 Nanyi mwajua, Sara mle ndani, akisikiliza kisiri, kwa namna fulani ana hisia ya kukasirika nusu kutokana na hali yake asubuhi hiyo, akawazia moyoni mwake, "Sasa, hilo si ni jambo la kipumbavu? Wazia, katika siku zetu, mimi ni mwanamke mkongwe, kadiri nilivyo na umri mkubwa, mimi hapa umri wa miaka tisini, huyo hapo mume wangu Ibrahimu ameketi, mwenye umri wa miaka mia moja! Vema, mimi, halijatukia kwangu kama wanawake kwa miaka hamsini. Naye Ibrahimu, vema, tumekuwa katika ndoa tangu tulipokuwa na umri wa kama miaka kumi na saba, naye akiwa na umri wa kama miaka ishirini na saba, vema, hilo li—lingewezekanaje? Lingewezekanaje?"

84 Mnaona, mwenyewe hakuwa katika hali ya kuipokea wakati Mungu alipoileta. Loo, jamani, kamwe usiingize hilo moyoni mwako, kuwa wazi, kuwa tayari. Aliikosa, akashindwa kuiona. Mimi . . . Labda, tusipokuwa waangalifu, enyi marafiki, kanisa litakosa kuiona. Hebu tusitafute mitindo ya nywele ya kanisa na nguo mpya, hebu tumtazamie Roho Mtakatifu kuja katika mambo ya kimbinguni na kuinua mambo fulani.

85 Kanisa halihitaji kufanyiwa marekebisho, linahitaji kuzaliwa, Roho Mtakatifu kuingia kanisani, kuwarudisha watu, na, wanaoamini mambo ya kimbinguni, na kushikilia na

kungojea kule Kuja kwa Bwana, kana kwamba inaweza kuwa saa yoyote, kuishi katika hali hizo.

86 Huyu hapa katika hali hiyo, akisema, "Sasa, hilo lingewezaje kutukia katika wakati wetu wa kisasa? Ingewezaje kunipata katika hali yangu?" Lakini ilitukia vivyo hivyo.

87 Ibrahimu, huko nje, akingojea kwa hamu, mnaona, hakujulishwa, walijulishwa wale waliokuwa wakiitazamia. Hivyo ndivyo inavyokuja bado, kwa wale wanaotazama. Kwa hiyo, alikuwa akiangalia, Ibrahimu alikuwa akiangalia. Akasema, "Naam, Bwana wangu. Naam, hiyo ni kweli, ahadi ilikuwa, na—nami nimeiamini wakati wote."

88 Akasema, "Sasa, Ibrahimu, yapata tu muhula wake, itakuwa ni kila mwezi, vema, nitakurudia, nawe utampata mtoto huyo."

89 Naye Sara, mwajua mwenyewe, akasema, "*Humph*!" akacheka kimoyomoyo. Sasa angalieni, Ibrahimu anapata ishara sasa. Mnaona, Sara alikuwa amefadhaika sana, anajali sana—sana kuhusu mtindo mpya wa nywele aliouona, ama—ama kitu kingine.

90 Wakati mwingine tunafadhaika sana juu ya jamaa huyo, jamaa huyo mwingine aliye na madhehebu makubwa kuliko yote, ama, "Kusanyiko lake linavalia vizuri kuliko langu." Ama, "Wana kanisa kubwa huko chini pembeni kuliko tulilo nalo." Hiyo inaleta tofauti gani? Ninamtaka Mungu, sijali kama itanibidi kumwabudia pembeni mwa barabara, katika kibanda cha makaa ya mawe, popote pale, ninamtaka Mungu. Jalia moyo wangu uwe katika hali nzuri, kama nikivaa ovaroli, mradi ninaweza kumwangalia Mungu na kuona hatua Yake na kumtambua Yeye, sio kuipita.

91 Akasema, "Ibrahimu, yu wapi Sara, mkeo?" Mgeni, hajawahi kumwona hapo kabla, "Yu wapi Sara, mkeo?" Basi alijuaje kwamba alikuwa na mke? Tena alijuaje ya kwamba jina lake lilikuwa ni Sara?

Kasema, "Yuko hemani nyuma Yako."

92 Basi Sara alipocheka, Yeye alisema, "Kwa nini akacheka?" Alishika ile ishara, alijua ilikuwa ni nini. Sara hakulipata, hata alijitokeza na kujaribu kulikanusha. Mungu angalimwangamiza kwa hilo kama asingalikuwa sehemu ya Ibrahimu.

93 Na mara nyingi kutokuamini kwetu kungetuangamiza kama si Damu ya Yesu Kristo. Mungu hawezi kutuangamiza sasa kwa sababu Damu ya Yesu Kristo inamweka Mungu mbali nasi. Sisi ni sehemu ya Kristo, kama tu vile Sara alivyokuwa sehemu ya Ibrahimu, kwa kuwa sisi ni Bibi-arusi wa Kristo. Nasi watu tuliozaliwa na Roho wa Mungu, tunapaswa kuamka, tutoke kwenye hamaki zetu, na kuangalia ishara ya kimbinguni ya Kuja kwa Bwana Yesu, ishara Zake alizoahidi.

94 Kumbukeni, Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, alisema jambo lilo hilo lingejirudia tena, "Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika kuja Kwake Mwana wa Adamu," kwamba Mungu angekuwa akifanya kazi kupitia mwili wa mwanadamu, akifanya jambo lile lile alilofanya wakati huo. Ee Mungu, tusaidie kuamka! Siku ya kujiliwa imewadia.

95 Unasema, "Loo, Mungu hawatumi Malaika, tena."

96 Roho Mtakatifu ndiye Malaika huyo, Roho Mtakatifu ndiye Mtu huyo. Roho Mtakatifu, Yesu alisema Yeye, Roho Mtakatifu, atakapokuja, atafanya kazi alizofanya, Yeye angekuwa pamoja nasi, hata ndani yetu, na angetukumbusha mambo ambayo alikuwa amefundisha, na angetuonyesha mambo yajayo, "Kazi nizifanyazo Mimi, yeye naye atazifanya." Sasa, tunaishi katika siku hiyo. Tunaishi katika huo wakati.

97 Angalieni: "Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma." Lakini mnajua nini? Hilo tabaka jingine la watu huko chini Sodoma halikupata ishara hiyo, kundi tu lililoitwa litoke ndilo lililopata ishara hiyo, wale tu waliolitambua, wale waliolielewa. Hivyo ndivyo ilivyo siku hizi, Roho Mtakatifu akifanya kazi Zake. Makundi makubwa makubwa ya watu na umati wa ulimwengu, na inakuwa Sodoma na Gomora ya kisasa, mnajua ndivyo ilivyo.

98 Mbona, nilisoma kwenye—kwenye gazeti hapa, huko Los Angeles, hapa wakati fulani uliopita nilikuwa nikiruka juu ya Los Angeles, na kuona kwamba ulawiti ulikuwa ukiongezeka kwa asilimia arobaini zaidi ya mwaka uliotangulia; wanaume wakiwachukua wanaume chumbani na kuishi nao kama wake zao, upotovu. Hivyo ndivyo dhambi ya Sodoma ilivyokuwa, hasa na hicho ndicho kitu tulicho nacho. Hata serikali yetu imejaa hao, taifa zima limezingirwa nao, ukomunisti, kila kitu kikiuvunja.

99 Anayeliua tofaa si robini anayelidonoa, ni mdudu aliye kwenye kiini chake. Siogopi Ujerumani, ama baadhi ya mataifa haya mengine, ni uozo wetu wenyewe miongoni mwetu, kumwacha Mungu ndiko kunakoliua taifa hili, kunaliozesha. Baridi, utaratibu, kuingia katika makanisa yaliyojazwa na Roho kunalipoozesha, hicho ndicho kitu kitakachotuua, sio tu kutafuta kitu fulani hapa, kitu fulani cha ulimwengu, na kazi kubwa, na starehe, na ahadi kubwakubwa, na mambo haya yote ya namna hii, ondoa macho yako kwenye hayo. Zindukia ukweli kwamba Mungu angali ni Mungu, Naye ni Mungu yeye yule aliyeahidi hizi ishara. Haleluya! Ninaamini Yeye yupo hapa. Mnaamini hilo?

Na tuinamishe vichwa vyetu.

100 Baba wa Mbinguni, Wewe ni Mungu, Mungu wa milele, nami ninanukuu Maneno ya Mwanao mpendwa. Alisema kama ilivyokuwa huko chini siku ile huko Sodoma, kabla tu ya Moto

kushuka kutoka Mbinguni na kuuangamiza huo mji, ndivyo itakavyokuwa katika kuja Kwake Mwana wa Adamu.

101 Sasa, Baba, tunaona kule, yametundikwa kwenye mabanda, mabomu ya atomiki, yamewekwa huko visiwani, mabomu ya atomiki, mabomu ya haidrojeni ambayo yatalipua shimo ardhini lenye kina cha futi mia moja na hamsini kwa maili mia moja mraba, maelfu ya hayo yameelekezwa kwenye kila taifa. Nyambizi zikizunguka-zunguka chini ya maji, matetemeko ya ardhi sehemu mbalimbali, visahani virukavyo angani, mambo ya kutisha katika mbingu juu, mioyo ya watu ikivunjika, fadhaa ya wakati, dhiki kati ya mataifa.

102 Ee Mungu, halafu Wewe huyu hapa unakuja, ukitenda kazi jukwaani pamoja na Roho Mtakatifu, akivuta kanisani, akizileta siku za Sodoma. Tunaona roho ya Wasodoma. Wanawake mitaani, makanisani, wakivalia kizinifu, wakivaa kila namna ya nguo za kizinifu, zilizovaliwa zipate kumjaribu mwanaume mitaani, wamepagawa pepo wachafu wala hawajui.

103 Wanawake wazuri wakizipeleka nafsi zao kuzimuni nao watawajibika kwenye Siku ya Hukumu kwa kufanya uzinzi, ingawa yeye ni safi kama yungiyungi, kimwili, lakini amejianika mbele ya wanaume, "Kila mtu amtazamaye mwanamke kwa kumtamani amekwisha kuzini naye moyoni mwake." Huku mwanamke huyo hajui ya kwamba akivaa namna hiyo na mwanamume akimwangalia, itambidi kuwajibika kwa kufanya uzinzi, kwa kuwa alijiruhusu kuvaa hivyo, kisha akaketi mbele ya wanaume apate kumjaribu.

104 Mungu, liangalie taifa hili, Bwana, liangalie kanisa, jinsi lilivyomeza upuuzi huo, ninii tu, wa Shetani, kwa urahisi tu. Naye Shetani amewalisha uharibifu huu wa kuzimu, na maelfu mengi wameuamini.

105 Loo njoo, Bwana Yesu, njoo Bwana. Ulisema kama kazi haikufupishwa, hakuna mwenye mwili atakayeokolewa. Kweli Bwana, tunaona hilo ndani yetu siku hizi, tunaona kule kuanguka na kupoa. Jalia masalia walioponyoka kutoka Babeli hii, na wainuke na kuangaza, naomba uwajaze kwa nguvu za Mungu, Roho Mtakatifu aje juu yao, Bwana, na kutenda zile kazi kuu za Mungu, na kuwavuta wale waliokusudiwa Uzima wa Milele warudi zizini tena. Tujalie, Bwana, tujalie, yasikie maombi yetu.

106 Watu wameketi hapa usiku wa leo, tutafanyiza mstari huu wa maombi katika dakika chache, nao watu watapitia mstarini. Ninaomba Baba, ya kwamba Wewe utawaamsha watu, kuwafanya wajue ya kwamba tunaishi katika, kitu kama Sodoma na Gomora mamboleo. Tujalie, Bwana, ya kwamba wataona ya kwamba yule Malaika aliyeahidiwa kutuzuru, kupitia mwili wa binadamu . . .

107 Na Bwana, tunajua ya kwamba Malaika huyo ni Mjumbe kutoka Mbinguni ambaye ni Roho Mtakatifu, ni Yeye, anayetaka kufanikisha kupitia sisi mapenzi ya Mungu, kuliita Kanisa. Tujalie, Bwana. Mtume tena usiku wa leo, mtume yule Elohimu mkuu aliyeshuka mavumbini na kujitambulisha Mwenyewe, kwa sababu angeweza kuzungumza na mwanadamu kupitia mavumbi. Tumia mavumbi yaliyo humu ndani, Bwana, yaliyowekwa wakfu Kwako, mavumbi haya yaliyotakaswa kwa Damu ya Yesu, yatumie, Bwana.

108 Jalia, kama kuna asiyeamini hapa Bwana, na waone ya kwamba ile saa inakaribia. Wanayaona kwenye magazeti, wanayasikia kwenye redio na televisheni, sasa jalia waone ishara ya Mungu, kwamba Yeye analiita Kanisa Lake, akilipa ule wito wa mwisho, wa kumalizia, ile ishara ya mwisho, ya kumalizia ambayo lingepokea. Tumekuwa na uponyaji, na kunena kwa lugha, na miujiza, na kadhalika, lakini kujiliwa huko ndiko tunakotazamia usiku wa leo, Bwana. Tujalie. Katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

109 Samahani, niliwapeleka muda mrefu sana. Ndugu, dada, mimi ni bonge tu la udongo, msiniangalie mimi, ila sikilizeni nisemacho. Kuja kwa Bwana kunakaribia. Sijui kuko karibu kiasi gani, hakuna ajuaye, lakini ninaamini kuko karibu sana, ninaona kila kitu kikitendeka tu. Ninawatakeni muwe tayari, ninawatakeni mfunguliwe kabisa na . . . "Wekeni kando kila dhambi, kila mzigo, na dhambi ile inayowazinga kwa upesi, mpate kupiga mbio kwa saburi katika yale mashindano yaliyowekwa mbele yetu, tukimtazamia Mwenye kuanzisha na Mwenye kutimiza imani yetu, Yesu Kristo."

110 Angalieni ninii Yake—angalieni upole na unyenyekevu Wake, angalieni fadhili na rehema Zake, angalieni Roho Wake akirudi duniani. Hilo linathibitisha ya kwamba Yeye yu hai, hajafa. Wasingeweza hata kuuua huo mwili, waliuua, kweli, bali Mungu akaufufua tena, na yu hai milele, ameketi mkono wa kuume wa Mungu. Roho aliyekuwa ndani yake yuko hapa kanisani usiku wa leo, aliahidi jambo hilo. Tuko katika wakati wa mwisho.

111 Sasa, sikumbuki tu mahali tulipoachia hivi majuzi usiku, kuita hizi kadi za maombi, tulikuwa tumebakisha zingine. Tuliita baadhi yake halafu ninii . . . [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

112 Amina. Amina. Na iwe hivyo. "Mungu hufanya kazi kwa njia za ajabu, kufanya maajabu Yake."

113 Kumbukeni, Roho Mtakatifu aliyekiandika Kitabu hiki, Roho Mtakatifu aliyekuwa katika yale mavumbi huko chini Sodoma, ndiye Roho Mtakatifu yule yule aliye katika jengo hili usiku wa leo, Yeye anaweza kufanya jambo lile lile. Mnaamini hilo? "Kama unaweza kuamini, yote yanawezekana."

114 Ninawatakeni mwombe, kwa kuwa ni—ni—ninajikwaa nikitafuta maneno, mimi. . .Ananitaka nifanye jambo fulani, sijui ni nini. Kwa hiyo ombeni tu pamoja nami, na halafu Bwana anajaribu kufanya jambo tofauti, sijui ni nini. Iweni tu na kicho, na kila mtu aketi tu kitini mwake. Iweni tu. . .Hatujui nini, jambo fulani linaweza kutukia hapa katika dakika moja. Sijawahi kuwa na hili hapo kabla, namna hii tu. Iweni tu katika maombi, na Bwana Mungu na atufunulie.

115 Naam, hili hapa: Nitageuza mgongo wangu kuelekea kusanyiko hili, kuwafanya mjue ya kwamba Malaika yeye yule aliyekuwa kule Sodoma, aliyetoa ishara hiyo huku amegeuza mgongo Wake, ndiye Malaika yule yule aliye hapa usiku wa leo, si ndugu yenu, ni Bwana wenu, Roho Mtakatifu.

116 Sasa, ninyi watu katika sehemu hizi za makanisa haya hapa usiku wa leo, sisemi itakuwa hivyo, Kitu fulani kilinifanya nifanye hivi, lakini kama Roho Mtakatifu atakuja hapa katika jengo hili, na kutenda, na kufanya tu kama alivyofanya kule Sodoma, kwa Kanisa teule, watu walioitwa watoke, waliotengwa na kundi hilo la watu kule chini. . .Hapo ndipo alipokuja: Ibrahimu. Wale—wale Malaika, wajumbe, walishuka wakaingia Sodoma na kuhubiri, lakini Huyu alibaki nyuma, kwa Kanisa, Kanisa lililoitwa litoke, Naye akawapa ishara kwamba Yeye *alikuwa*.

117 Sasa, kama Roho Mtakatifu atafanya hivyo, nawe utaomba moyoni mwako na kumwamini Mungu, useme, "Mungu, mimi ni mwana wa Ibrahimu, nami ninaamini kwa moyo wangu wote," basi hebu Roho Mtakatifu aje na kutenda hapa usiku wa leo, kama alivyotenda kule chini, je, ninyi nyote mtamwamini Yeye, kwa moyo wenu wote?

118 Hebu tuninii tu, kwenye piano, yeyote aliye mpiga piano hapo, tafadhali, imba *Nanii Mkuu*. . .cheza tu polepole, *Tabibu Mkuu Sasa Yu Karibu,* tafadhali, huku tukiomba tu. Sasa, hili ni la kiroho.

119 Ninakumbuka wakati fulani uliopita, huo ulikuwa ukicheza, Fort Wayne, Indiana, jambo fulani likatukia, msichana wa Dunkard ambaye hakuwa na Roho Mtakatifu, akajazwa na Roho, kisha akaruka kutoka kwenye piano, akakimbia, yapata watu elfu tano walioketi pale waliona piano hiyo ikiendelea kucheza, *Tabibu Mkuu Sasa Yu Karibu*. Watu wakiinuka tu kila mahali, wakiponywa. Lilikuwa ni kundi la Waamishi na Wadunkardi, Fort Wayne, "Yesu mwenye huruma."

120 Nitawaangalia ndugu zangu hapa nyuma. Ninyi ombeni.

121 Ndugu, sote tutakutana siku moja huko kwenye Nchi iliyo ng'ambo. Nasi itatubidi kutoa hesabu kwa ajili ya huduma zetu, yale tunayofanya na Yesu, aitwaye Kristo. Tunawafundisha watu wetu ya kwamba Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele. Mnaamini hilo, sivyo ndugu?

122 Sasa, sasa hebu kidogo, kuna mtu upande wangu wa kulia kabisa, anaomba. Ni mwanaume. Naye anaomba, kwa sababu yuko katika hali mbaya, anaugua, kitu kama ugonjwa wa kibofu, ana uvimbe. Amefanyiwa upasuaji. Na ni . . . Anangojea upasuaji mwingine. Huyo ni huyo mtu aliyeketi papo hapo ameinua mkono wake. Hiyo ni kweli. Kama hiyo ni kweli, simama kwa miguu yako. Kama hatufahamiani, punga mkono wako.

123 Unaamini Malaika yeye yule wa Mungu yuko humu jengoni?

124 Mungu akubariki, ndugu. Kubali . . . Uligusa nini, bwana? Ulikuwa ukiomba, sivyo, kwa ajili ya uponyaji wako? Vema basi, kama mimi nikisimama hapa, nimekuelekezea mgongo, Malaika yule yule aliyetangaza jambo hili huko Sodoma, ambaye Yesu alisema angekuwa hapa katika siku za mwisho, kabla tu ya Kuja Kwake, basi jamani, Yeye yuko njiani Mwake akija hapa, anakuja, hiyo ni kweli. Ombeni.

125 Sasa, aliyeketi karibu naye, moja kwa moja nyuma yake ni mwanamke, ana shida na ubavu wake, naye anaumwa na kichwa. Bibi Arnold, kama unaamini kwa moyo wako wote! Vema. Sikujui wewe. Hiyo ni kweli, mama? Hivi hatufahamiani? Hilo ndilo jina lako? Huo ndio ugonjwa wako? Ulikuwa unaomba, sivyo? Uligusa Kitu fulani.

126 Huyo mtu aliyeketi moja kwa moja huko nyuma akiwa na shinikizo kuu la damu, kama utaamini, bwana, utaukubali kama uponyaji wako? Unaukubali? Unayeniangalia, mwenye mvi, bwana . . .? . . . amini kwa moyo wako wote. Unaamini bwana? Vema, basi hilo shinikizo la damu litakuacha.

127 Simjui, sijawahi kumwona maishani mwangu. Hiyo ni kweli, bwana? Inua mkono wako kama hatufahamiani. Hao watu wanagusa nini?

128 Na katikati ya haya yote, ninahisi shaka ikiingia. Kwa nini mnafanya hivyo? Mungu aturehemu! Msifanye hivyo. Roho Mtakatifu yuko hapa, BWANA ASEMA HIVI.

129 Ninaona mbele yangu, mwanamke, amemshika mtoto mchanga mwenye kichwa kilichojawa maji. Mtoto huyo amefanyiwa upasuaji, ana maji kwenye ubongo. Ameketi papa hapa chini, amemshika huyo mtoto mchanga. Mnajua ninazungumza na nani? Bibi Yeager, simama, na uamini kwa ajili ya mtoto huyo mchanga.

130 Unamwamini Bwana? "Kama unaweza kuamini!" Vipi kuhusu sehemu hii hapa? Ili kwamba mtaona, inakaa tu katika sehemu moja . . . Wewe amini hapa. Unaamini hilo?

131 Mama aliyeketi hapa, shinikizo kuu la damu, kama utaamini, mama . . . Bwana, yeye ni nani? Bi. B-i-r-l-e-y. Birley, amini kwa moyo wako wote, nawe utapata uponyaji wako, pia. Unaliamini? Vema.

132 Vipi kuhusu mwanamke huyu aliyelala hapa kwenye kitanda hiki cha wagonjwa, machela? Angalia upande huu, mama. Una kadi ya maombi? Nakisia huna. Vema, si—sidhani. . .Nilisahau kuwaambia kuhusu kadi za maombi, nadhani, hakuna mmoja wenu. . .Huna kadi ya maombi? Siwezi kukuponya, mama. Lakini unaamini kama Mungu anaweza kuniambia shida yako ni nini, utaukubali? Utakufa umelala hapo, hilo ni jambo moja la hakika. Una mwili uliojaa maji kupita kiasi, huo ni ugiligili, na kadhalika, ukikusukuma. Hiyo ni. . .? Hiyo ni kweli, sivyo? Sasa, sijawahi kukuona maishani mwangu. Hii ndiyo mara ya kwanza, na kama utaamini kwa moyo wako wote wala usitie shaka, ugiligili huo utakuacha, nawe utaenda nyumbani, uwe mzima. Amina.

133 Mnaamini? Mnaamini Malaika wa Bwana yupo hapa? Ni wangapi wenu walio waaminio? Inua mkono wako. Vema, sasa wekeaneni mikono, wekeaneni mikono kama ninyi ni waaminio.

134 Ee Mungu, Roho Mtakatifu aliyepo, yule Malaika aliyeahidiwa, ambaye Yesu alisema angekuwa hapa kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, Bwana Mungu, mfanye Shetani awaache watu hawa. Ninawashikilia mbele Zako, na nina bidii juu yao.

135 Toka kwenye kundi hilo, Shetani, katika Jina la Yesu Kristo, toka kwa watu hao na utolewe kwenye jengo hili!

136 Naye Yesu Kristo atwae utukufu na nguvu, milele.

137 Sasa, kama unamwamini kwa moyo wako wote, amini ya kwamba Yeye anakuponya, Biblia ilisema, "Hizi. . . "

138 Hilo ni sawa, mama, simama moja kwa moja kutoka kwenye kitanda hicho na uende nyumbani, hivyo ndivyo ilivyo.

139 Mnaamini? Simameni kwa miguu yenu basi, kila mahali, mkubalini Yesu. Malaika wa Bwana yupo hapa. Ninatangaza baraka za uponyaji na nguvu za Mwenyezi Mungu mikononi mwenu. . .?. . .

60-0328 Kuna Jambo Lolote Lililo
Gumu Sana La Kumshinda Bwana?
Municipal Auditorium
Tulsa, Oklahoma Marekani

SWAHILI

©2026 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org